



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 1/11/2023

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA AJILI YA UJENZI CHUMBA
KIMOJA CHA DARASA SHULE YA MSINGI LUPOTO

ZABUNI NA:LGA/071/2023/2024/RDC/W/17

1. **Mkurugenzi Mtendaji (W)** anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imetoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa **Chumba Kimoja cha Darasa Shule ya Msingi Lupoto** itakayojengwa katika Kata ya Kyimo kupitia **Fedha za Mapato ya Ndani** kwa Mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Ujenzi wa Miundo mbinu katika Shule hiyo utahusisha ujenzi wa **Chumba Kimoja cha Darasa**
3. Hivyo basi, Mkurugenzi Mtendaji (W) anakaribisha Mafundi ujenzi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kuomba kazi za Ufundi kwa utaratibu wa "**Force Account**" katika fani na sifa za Ufundi zifuatazo:-

1.Fundi Uashi

- I. Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi na mwenye kujua kusoma ramani za majengo.
- II. Awe na vitendea kazi za kunyoosha ukuta kama vile Square, bridge (Plumb Bob), mwiko, Komabao, Pima maji n.k
- III. Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani

2.Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).


- I. Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
- II. Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

3.Fundi Aluminium

- i. Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani.
- ii. Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

4. **Pamoja na sifa zilizotolewa hapo juu waombaji wanapaswa kuzingatia masharti kama ifuatavyo:-**

- I. Awe Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
 - II. Awe na Namba ya Utambulisho wa mlipa kodi (TIN) (aambatanishe na barua ya maombi kwa uthibitisho zaidi)
 - III. Awe na akaunti ya benki kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe.
 - IV. Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa anakoishi.
 - V. Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi mradi utakapokamilika
5. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu **ziwasilishwe ofisi ya Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi Lupoto, S.L.P 148, Tukuyu** yakiwa yamefungwa kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi ya Ufundi unaoombwa mfano **Ufundi Uashi n.k**
6. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi za ufundi ni siku ya Jumanne ya Tarehe **07/11/2023** kabla ya saa 5:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.
7. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi utakaofanyika tarehe **07/11/2023** saa 6:00 Mchana utakaombatana na kuwashindanisha nukuu za bei za ufundi.
8. Wako katika ujenzi wa Taifa



Mchau, R.B

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE**